**THE UNITED REPUBLIC OF TANZANIA**
**NATIONAL EXAMINATIONS COUNCIL**
**CERTIFICATE OF SECONDARY EDUCATION EXAMINATION**

**015/2** **ELIMU YA DINI YA KIISLAMU 2**
(Kwa Watahiniwa Walioko na Wasiokuwa Shuleni)

**Muda: Saa 2:30** **Jumatano, 13 Novemba 201 3 mchana**

**Maelekezo**

1. Karatasi hii ina sehemu A, B, C na D.
2. Jibu maswali **manne (4)**, swali **moja (1)** kutoka kila sehemu.
3. Kila swali lina alama 25.
4. Simu za mkononi **haziruhusiwi** katika chumba cha mtihani.
5. Andika **Namba yako ya Mtihani** katika kila ukurasa wa kijitabu chako cha kujibia.



Find more free educational resources at http://maktaba.tetea.org
Scanned by CamScanner

## BISMILLAHIR - RAHMANIR - RAHIIM

## SEHEMU A: QUR'AN

1. Andika tafsiri ya Suratu-Takaathur, kisha elezea vipengele vitano katika kubainisha ujumbe utokanao na sura hiyo.

2. Eleza maana ya "Al-Mu'awwidhatain na kisha chambua shari sita tunazojikinga kwa kusoma Al- Mu'awwidhatain.

3. Bila shaka Waislamu wanaamini kuwa Qur'an ni kitabu cha mbinguni kilichoteremshwa kutoka kwa Allah (s.w) kuja kwa Nabii Muhammad (s.a.w) na si utunzi wa Muhammad (s.a.w) ili kuwania ukubwa na madaraka. Thibitisha kauli hii.

## SEHEMU B: TAWHIID

4. Na anayetaka dini isiyokuwa ya Kiislamu basi haitakubaliwa kwake. Naye Akhera atakuwa katika wenye khasara (kubwa kabisa) (3:85). Toa hoja sita kuonesha kuwa Uislamu ndio dini sahihi.

5. Eleza hoja sita kudhihirisha kuwa historia ya Mitume wote ni dalili ya kuwepo Mwenyezi Mungu.

6. Jadili kazi sita za Malaika na jinsi kila kazi inavyomfanya muumini kuwa mcha Mungu.

## SEHEMU C: FIQH

7. *Chukua Sadaqa katika mali zao, uwasafishe na kuwatakasa kwa ajili ya hizo (sadaqa zao) na kuwataja kwa vizuri (mbele Yangu) na uwaombee dua (9:103).* Eleza mambo manne yanayoonesha utakaso unaotokana na utoaji wa Zakat na Sadaqat.

8. Kwa kuzingatia Funga ya mwezi wa Ramadhani, toa maelezo mafupi juu ya:
   (a) Futari na Daku
   (b) Itiqaf
   (c) Lailatul-Qadr
   (d) Zakatul-Fitri
   (e) Idd el-Fitri

9. Eleza aina sita za biashara haram ambazo Muislamu amekatazwa kuzifanya.



Find more free educational resources at http://maktaba.tetea.org
Scanned by CamScanner

## SEHEMU D: TAREKH

10. Eleza kisa cha Nabii Lut (a.s) na mafundisho yake, kisha jadili mambo makuu matatu yaliyofanywa na watu wa Lut ambayo yanajitokeza katika jamii ya leo.

11. *Nasi hatukukutuma, (hatukukuleta) ila uwe rehema kwa walimwengu (wote) (21:107).*
    (a) Eleza kwa kuzingatia hali halisi ya enzi ya ujahiliya kero saba zilizotawala katika jamii.
    (b) Onesha kuwa Muhammad (s.a.w) ni rehema kwa binadamu.

12. Kuna mengi ya kujifunza kutoka katika historia ya Adam (a.s) na Ibilisi. Ainisha mafunzo nane kati ya hayo.



Find more free educational resources at http://maktaba.tetea.org
Scanned by CamScanner